Sura Ya Kwanza

UTAMBULISHO

Safari Kuelekea Uhuru wa Kifedha

Mambo yaliyo rahisi kufanya ndiyo hayo ambayo si rahisi kufanya - ***Jim Rohn***

Kabla ya kuanza kuangazia safari hii adhimu na muhimu katika maisha yetu, ningependa tuanze na fasili ya uhuru wa kifedha ili tupate mwanga zaidi.

Uhuru wa kifedha umefasiliwa na wataalamu wengi sana, ila ningependa kuazima fasili ya ndugu Jim Rohn ambaye anafahamika duniani kama mtaalamu wa maendeleo binafsi ambaye anasema, ***uhuru wa kifedha*** *ni uwezo wa kuishi kutokana na kipato cha rasilimali zako*. Hii ikimaanisha ili useme unahuru wa kifedha, ni lazima uwe na uwezo wa kupata fedha kutokana na vyanzo vyako mbalimbali vya kuingiza kipato ikiwamo uwekezaji na biashara.

Ni vyema nikasisitiza ya kuwa, uhuru wa kifedha hauna kiwango maalumu ili useme sasa umefika mwisho, bali vyanzo vyako viweze kukupatia kipato ambacho kitakusaidia wewe kuishi kwa uhuru bila kutegemea mtu mwingine kuishi maisha ya ndoto yako.

Nimependa kuanza na utambulisho huu wa safari kuelekea uhuru wa kifedha ili kutoa ujumbe kuwa safari

ni rahisi. Najua unaweza shangaa ninavyosema kuwa kufikia uhuru wa kifedha ni rahisi, ila naposema ni rahisi ni kwa sababu unaweza kufanya mambo yaliyo ndani ya uwezo wako bali unapaswa kufanya kazi kwa bidii, kujituma, kuwa muelewa, kuwa makini, kujitoa, kujifunza na kujinyima. Safari hii sio ngumu kama utafanya yale mambo yote rahisi kuelekea uhuru wa kifedha. Safari itakuwa ngumu sana endapo hutofanya yale mambo yote rahisi yanayohitajika. Kumbuka *mambo yaliyo rahisi kufanya ndiyo mara nyingi huwa sio rahisi kufanya.* Inawezekana nimekuchanganya kidogo katika kauli hii ila nitaifafanua zaidi kadiri tunavyoendelea kwenye kitabu hichi.

Tunaposema safari ya kuelekea uhuru wa kifedha, kumbuka safari hii ni ya kwako na sio ya mtu mwingine. Safari ya kutafuta uhuru wako wa kifedha haiwezi kuletwa na mtu mwingine bali wewe mwenyewe. Nia ya kuandika kitabu hichi, ni kutaka kukuonyesha yale niliyoweza kufanya mimi kuelekea uhuru huu wa kifedha na kukuonyesha wewe msomaji ya kuwa unaweza kufikia uhuru wa kifedha endapo safari hii utaianzisha wewe kufikia malengo yako.

Wengi wetu hupenda kujiuliza ni lini nitafikia uhuru wa kifedha? Na wakati mwingine hupenda kutizama watu mbalimbali waliofanikiwa na kutamani kuwa kama wao. Majibu ya kufikia uhuru wa kifedha yatapatikana kwenye kitabu hichi lakini pia kukupatia njia sahihi ya kufikia uhuru wa kifedha.

Kama niliovyosema hapo awali, ili kupata uhuru wa kifedha lazima safari hii iwe yako binafsi na utafute namna itakavyokuwa ya kipekee. Mara nyingi, tunapenda kujifananisha na wengine bila kujua safari zao na kufanya mambo kimakosa na badala ya kuwa na uhuru wa kifedha tunaishia kuwa na madeni mengi na ufukara mwingi.

Kama ilivyo kwa watu wengine wote, nilianza safari ya kutafuta uhuru wa kifedha bila kujua pakuanzia, nilidhani kama ilivyo kwa wengi kwa kuwa nimeajiriwa nitafanikiwa tu maishani. Zaidi ya yote, niliamini kwa kuwa nimepata elimu ya chuo kikuu nitafanikiwa tu. Nilipoona mambo hayaendi kadiri ya matarajio, nilidhani nahitaji mshahara mkubwa zaidi kufanikiwa. Bali kipato cha mshahara kilivyokuwa kinazidi kuongezeka, sikuona kama uhuru wa kifedha ulikaribia kwa namna yoyote ile. Maswali nayo yakazidi bila kujua pakuanzia, nikiangalia wengine waliofanikiwa bila kujua walifikaje hapo, nilibaki na imani iko siku nitafanikiwa na kuwa na uhuru wa kifedha. Kumbuka, imeandikwa katika Biblia Takatifu "*Imani peke yake bila matendo imekufa*" (Yakobo 2:14-26). Japokuwa nilikuwa na imani ya kufanikiwa sikujua nitafanikiwaje, kwani nilibaki njia panda bila kujua pakuanzia na nini cha kutenda.

Wakati nikiwa najiuliza maswali mengi, niliamini ya kuwa sifiki nilipopatarajia kwa kuwa maisha ni magumu hivyo siwezi kufanikiwa, pia nilidhani nimetoka kwenye familia maskini, lakini wakati mwingine nilidhani wale wote

waliofanikiwa walipata uhuru wa kifedha kwa kuwa walikuwa matapeli, wezi ama walidhulumu mali za watu. Kadiri nilivyoona mambo hayafanikiwi, niliamini kutokufikia kwangu malengo ni kutokana na ukweli kwamba mambo yaliyo nje ya uwezo wangu yalichangia kunirudisha nyuma. Hivyo, nikaona nisubiri bahati yangu labda siku moja nitafanikiwa. Katika subira yangu, niliamini ya kuwa ili nifanikiwe nahitaji kuwa na fedha kuyafikia malengo yangu, hivyo nikasema siku nikipata fedha nyingi nitaweza kujisimamia mwenyewe. Nikawa na imani ya kupata fedha bila kujua hizo fedha nyingi nazozitarajia nitazipata wapi.

Baada ya kuishi kwa imani na matumini kwa muda mrefu bila mafanikio niliyoyatarajia, nikaanza safari ya kujifunza ili nijue wengine walifanyaje nami nijifunze kutoka kwao. Kwa kuwa mimi ni mpenzi wa kusoma vitabu, nikaanza kununua vitabu vichache vinavyohusu mafanikio na kutumia muda mwingi kujifunza mkondoni kupata maarifa mbalimbali kutoka kwa watu waliofanikiwa na njia walizotumia. Baada ya kujifunza kwa muda mrefu, nikagundua nilishindwa kutumia rasilimali muhumu sana Mungu aliyonijalia bila kujua. Rasilimali ninayoizungumzia ni TABIA, ambayo si tu ninayo peke yangu la hasha kila mtu anayo.

Muda wote wakati nahangaika kutafuta funguo ya mafanikio, nilidhani ili mtu afanikiwe anahitaji FEDHA kufanikiwa na wengine walienda mbali na kusema ili

ufanikiwe unahitaji WAZO, ikimaanisha jambo au fikra bunifu. Kumbe wakati wote huo nilikuwa nahaingaika na mambo yaliyo nje ya uwezo wangu, huku nikishindwa kufanyia kazi jambo lilio ndani ya uwezo wangu kwani sikudhani TABIA yangu ni rasilimali kubwa sana itakayonifikisha kwenye uhuru wa kifedha. Tabia kwa muktadha wa kitabu hichi, inamaanisha mwenendo na mtizamo sahihi wa maisha ya mtu katika maeneo ya maendeleo binafsi, fedha na afya.

Natambua msomaji kwa sasa unaanza kujiuliza ni kwa namna gani tabia yako inaweza kukuletea uhuru wa kifedha? Na sitoshangaa kama utaanza kukata tamaa kwani ulichotarajia sicho unachokisoma kwa sasa. Nikutie moyo, endelea kusoma nawe utapata mwanga namna ambavyo tabia yako inaweza kukuletea uhuru wa kifedha kwa kadiri unavyotamani.

Hapo awali niligusia ya kuwa, *mambo yaliyo rahisi kufanya ndiyo hayo ambayo si rahisi kufanya*, sasa hapa ndo utaanza kupata mwanga ninaposema TABIA ni rasilimali kubwa sana linapokuja suala la uhuru wa kifedha.

Watu wengi, ikiwamo mimi hapo awali, nilidhani ya kuwa ili kufanikiwa na kupata uhuru wa kifedha nahitaji kufanya mambo makubwa na ya ajabu; ndio maana nilishindwa kuona tabia yangu kama sehemu muhimu ya mafanikio yangu. Siku nilipojifunza umuhimu wa tabia yangu, ikanipasa kubadilika na ndipo nilipoanza kuona mambo yakibadilika katika maisha yangu.

Safari yangu ya uhuru wa kifedha ilianzia hapa, huku nikifurahia kila hatua niliyokuwa naipitia mpaka kufika hatua ya kuandika kitabu hichi, ambacho kinalenga kuwashirikisha hatua nilizopitia kuweza kufikia uhuru wa kifedha.

Nipende kusisitiza ya kuwa, safari hii sijafika mwisho kwani ni safari endelevu na siku zinavyozidi kusonga mbele nazidi kujifunza na kuboresha TABIA yangu kwa kila hatua nayoifikia. Nisisitize kwamba, safari ya kufikia uhuru wa kifedha haina mwisho, kila mara unapofika lengo moja ni budi kuwa na lengo lingine kubwa zaidi unalolenga kulifikia. Hivyo, kitabu hichi ni mjumuisho wa mafunzo niliyojifunza na kuthibitisha ya kuwa inawezekana kufanikiwa kwa kuwa na TABIA sahihi kufikia uhuru wa kifedha.

Unapojiandaa kusoma sura ya pili, naomba nikupe siri ya mafanikio na siri ya kushindwa zinazotokana na tabia yako.

Siri ya Mafanikio: Tabia chache rahisi zilizofikiriwa vizuri zikarudiwa kila siku huleta mabadiliko kwenye malengo ya mtu. Mfano, kuweka akiba kila mara unapopata kipato bila kujali wingi ama uchache wa akiba unayoweka. Jambo la msingi ni muendelezo wa tabia ya kuweka akiba kila wakati unapopata kipato chako.

Siri ya Kushindwa: Kushindwa kufanya maamuzi sahihi kwa kujirudia kila siku husababisha kushindwa kufikia

malengo ya mtu. Mfano, unafahamu kuwa unapaswa kuweka akiba kila unapopata kipato chako, bali huweki akiba kwa kuwa unasubiri kipato chako kiongezeke. Kufahamu umuhimu wa jambo na kutolifanya hupelekea kushindwa kufikia lengo lako.

Hivyo basi, kati ya hizi siri mbili chagua kilicho rahisi kwako kufanya kuelekea uhuru wako wa kifedha.

Nihitimishe sura hii kwa kusema, "*Ufunguo* ***muhimu*** *kwa mafanikio ya maisha yako ni* ***wewe.***" Tafakari hili wakati ukiendelea kusoma kitabu hiki kwenye mfululizo wa sura zifuatazo.